# UDHIBITI UVUVI HARAMU NA ONGEZEKO MAVUNO YA SAMAKI

NA MWANDISHI WETU

CHIMBUKO la Siku ya Uvuvi Haramu Duniani ni wazo lililoibuliwa katika Kikao cha 39 cha Kamisheni ya Nchi za Mediterranean mwaka 2015.

Kikao hicho kilipendekeza kuwepo kwa siku ya kimataifa ya kudhibiti uvuvi haramu, uvuvi usiotolewa taarifa na uvuvi usioratibiwa.

Kamisheni hii ilipendekeza kutangazwa kwa siku hiyo ili kutoa uelewa wa umuhimu wa vita dhidi ya uvuvi haramu, uvuvi usiotolewa taarifa na uvuvi usioratibiwa. Pendekezo hili liwasilishwa na kuridhiwa katika Kikao cha 32 cha Kamati ya Masuala ya Uvuvi ya Shirika la Chakula Duniani (FAO).



Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayehusika na Uvuvi, Dk Rashid Tamatamah, anasema Desemba 2017, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika maazimio yake ya mwaka kuhusu uvuvi endelevu, ilitangaza rasmi Juni 5 ya kila Mwaka kuwa Siku ya Kimataifa ya Vita dhidi ya Uvuvi Haramu, Uvuvi Usiotolewa Taarifa na Usioratibiwa.

Tamatamah anasema, Juni 5 ilichaguliwa kwa sababu wakati azimio hilo linapitishwa, kulikuwa na Itifaki ya Kuzuia Uvuvi Haramu kwa kupitia bandari. Anasema Tanzania iliridhia itifaki hiyo iliyolenga kudhibiti uvuvi haramu na kuongeza kuwa, siku ambayo itifaki hiyo ilipitishwa ilikuwa Juni 5, hivyo UN iliona vyema tarehe hiyo iendelee kwa kuwa inahusu uvuvi haramu.

Anasema kwa kuwa Tanzania imeridhia itifaki hiyo na kuunga mkono Azimio la Umoja wa Mataifa dhidi ya Uvuvi Haramu, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imedhibiti uvuvi haramu kwa asilimia 80 katika maji baridi yakiwemo maziwa, mito na mabwawa.

Kadhalika, imedhibiti uvuvi haramu kwa asilimia 100 katika maji chumvi hususan Bahari ya Hindi ambako aina kubwa ya uvuvi haramu iliyokuwa ikitumika ni wa kutumia milipuko ya baruti.

"Uvuvi haramu ni dhana pana ambayo pamoja na kuhusisha matumizi ya nyavu zisizoruhusiwa, pia inahusisha kitendo cha mtu kuvua bila kuwa na leseni, kutumia chombo cha uvuvi ambacho hakijasajiliwa na utoroshaji wa samaki kwenda nje ya nchi," anasema Dk Tamatamah.

Pamoja na serikali kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti uvuvi haramu, anasema changamoto za matumizi ya makokoro, watu kuvua bila leseni na utoroshaji wa samaki kwenda nje ya nchi bado zipo japo kwa kiasi kidogo.

"Kabla ya mwaka 2017, hali ilikuwa mbaya sana, lakini mwaka 2018 idara kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, waliendesha operesheni mwaka mzima ikiwemo Operesheni Sangara katika Ziwa Victoria na Operesheni Jodari katika Bahari ya Hindi zilizofanikiwa kuondoa nyavu haramu," anasema na kuongeza: "Katika bahari tulikamata meli moja ya uvuvi Mtwara ya kutoka Vietnam na wahusika walifungwa."

Anasema tangu mwaka jana, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilianzisha Mkakati Shirikishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha ulinzi shirikishi.

"Baada ya kukamilika kwa zile operesheni, idadi ya samaki kwenye maziwa, bahari na mito imeongezeka kwa kiasi kikubwa."

"Miaka ya nyuma kabla ya operesheni ile, mavuno ya samaki Tanzania kutoka vyanzo vyote vya maji yalikuwa tani 350,000 hadi 360,000, lakini kwa mara ya kwanza mwaka 2019 zilifika tani 382,000 na mwaka jana tulifikia tani 497,000," anasema Dk Tamatamah.

Kuhusu idadi ya wavuvi waliopo nchini, anasema Tanzania ina wavuvi wanaotambulika 253,000 na wafugaji samaki 30,000. Anabainisha kuwa, kesi zilizopo mahakamani kuhusu uvuvi haramu haizidi 10 kwa kuwa wengi hulipa faini.

**MBUNGE WA CHONGA** Mbunge wa Chonga Salum Mohammed Shaafi (ACT-Wazalendo), anasema kuchoma nyavu za wavuvi si suluhisho kwa uvuvi haramu, bali serikali inapaswa kuwapatia mikopo wavuvi ili wanunue zana za kisasa za uvuvi zikiwemo boti za uvuvi, na pia iendelee kutoa elimu kuhusu athari za uvuvi haramu.

"Uvuvi umetoa ajira kwa Watanzania, hivyo ni jukumu la serikali hasa ni kutoa elimu ili wananchi waondokane na uvuvi haramu unaoharibu mazalia ya samaki, unaoharibu utalii kwa kuwa bahari na maziwa ni sehemu ya vivutio vya utalii," anasema Shaafi.

**KUHUSU MIKOPO** Anasema mwaka 2018 lilianzishwa dawati la sekta binafsi ili wavuvi waweze kukopesheka na kabla ya 2018 kulikuwa hakuna mtu yeyote au kikundi chochote kilichopata mkopo benki, lakini mpaka Aprili mwaka huu, kuna vikundi ambavyo vimepata mkopo kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB).

"Kwa mfano, Ukerewe kuna akina mama wanaofanya kazi ya kuanika dagaa ambao ni tatizo kuanikwa wakati wa masika, tukawaunganisha na kusaidia kuwaandikia pendekezo na kulipeleka Benki ya TADB na walipata mkopo wa Sh milioni 200 walizotumia kununua mashine kwa ajili ya kukaushia samaki. kikundi kingine kinaitwa Iragula kilichopo Sengerema ambao walinunua boti za kuvulia na nyavu," anasema Dk Tamatamah.

**WAZIRI MIFUGO NA UVUVI** Wakati anawasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Wizara yake kwa mwaka 2021/2022 bungeni hivi karibuni, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema katika mwaka 2020/2021, Sekta ya Uvuvi nchini ilikua kwa asilimia 6.7.

Pia mchango wa sekta hii kwa pato la taifa ulikuwa asilimia 1.71 na kutoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi 195,435, wakuzaji viumbe maji 30,064 na Watanzania milioni 4.5 wameendelea kupata mahitaji yao ya kila siku kutokana na shughuli mbalimbali zinazohusiana na sekta ya uvuvi.

Ndaki anasema shughuli za wavuvi wadogo huchangia asilimia 95 ya samaki wote wanaovuliwa nchini na asilimia tano iliyobaki huchangiwa na wavuvi wakubwa.

Anasema hadi Aprili mwaka huu, wavuvi wadogo 195,435 walishiriki moja kwa moja shughuli za uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi 58,231 na kuvuna tani 422,859.8 za samaki zenye thamani ya Sh trilioni 2.62.

"Kulingana na taarifa za utafiti katika Ziwa Victoria mwaka 2020, kiasi cha samaki katika ziwa hilo kimeongezeka kutoka tani milioni 2.7 mwaka 2019 hadi tani milioni 3.5 kwa ziwa zima ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 29.3. Ongezeko hili limechangia kiasi cha samaki kilichopo katika maji yote kufikia tani milioni 4.1," anasema Ndaki.

Scanned with CamScanner

# Waziri Ndaki afunguka mafanikio Wizara ya Mifugo na Uvuvi siku 100 za Samia

NA MWANDISHI WETU



SIKU 100 tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarani zimekuwa za mafanikio makubwa katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwani katika kipindi hicho imetekeleza kazi mbalimbali.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki anasemaa kazi hizo ni zile zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha, Waziri Ndaki anasema baadhi ya kazi hizo zimetokana na maelekezo ya Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa katika matukio mbalimbali ili kuboresha Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Hivyo haya ni baadhi ya mafanikio ambayo yamepatikana katika siku 100 za utawala wa Rais Samia kama yanavyoelezwa na Waziri Ndaki.

TEKELEZAJI KATIKA SEKTA YA MIFUGO

Waziri Ndaki anasema katika kipindi cha siku 100 ya Serikali ya Awamu ya Sita, mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya mifugo ni pamoja na ujenzi wa visima virefu viwili (2) katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa (Usolanga) na Mpapa (Manyoni) vimefikia asilimia 70 na asilimia 30 mtawalia. Pia, ukarabati wa mabwawa matatu (3) ya Chamakweza (Chalinze), Kimokoua (Longido) na Narakauo (Simanjiro) umekamilika kwa asilimia 100.

Anaeleza mafanikio mengine ni kwamba jumla ya hekta 32,044.21 zimetengwa katika Wilaya za Tanganyika, Nsimbo na Mlele kwa ajili ya malisho.

Vile vile Waziri Ndake anafafanua zaidi katika kipindi hiki Serikali imetoa mafunzo na leseni kwa wachunaji ngozi 340 wa machinjio za Manispaa ya Kinondoni na Temeke Dar es Salaam.

Pia, imewapatia vitendea kazi Wakaguzi wa Ngozi 34 wa Wilaya za Mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga na Mara. Lengo ni kuwezesha upatikanaji wa ngozi bora kwa ajili ya viwanda.

"Mnada wa mifugo wa mpakani wa Magena, Mara umefunguliwa ili kuwezesha biashara ya mifugo kati ya Tanzania na Kenya. Pia, ujenzi wa mnada wa mifugo wa upili wa Buzirayombo, Geita umefikia asilimia 50. Lengo ni kuboresha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi," anasema Waziri Ndaki na kuongeza.

"Jumla ya ng'ombe wa asili 146 katika mkoa wa Iringa na ng'ombe 152 katika mkoa wa Singida walifanyiwa uchambuzi ili kubaini na kutunza mbari za ng'ombe wa asili."

Kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) zimefanya kikao na kukubaliana kuendeleza ushirikiano kiutendaji katika ngazi za idara na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo.

"Lengo ni kuimarisha sekta za mifugo katika pande mbili za muungano ili ziweze kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi."

TEKELEZAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI

Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi Waziri Ndaki anasema ni moja kati ya sekta za kiuchumi hapa nchini.

Anasema shughuli za uvuvi huchangia katika kuwapatia wananchi uhakika wa chakula, lishe, kuongeza kipato, kupunguza umaskini, kupata fedha za kigeni na kuchangia kwenye pato la Taifa.

Anataja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika siku 100 za uongozi wa Awamu ya Sita kuwa ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Majengo Matatu ya Ofisi za Vikundi vya usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi (BMU) katika Wilaya za Pangani (Kipumbwi), Mkinga (Zingibari) na Bagamoyo (Dunda).

Anafafanua kwamba ni katika kipindi hiki ambapo kumekuwa na juhudi za maboresho ya miundombinu wezeshaji ya shughuli za uvuvi kwa kuanza ujenzi wa mialo sita (6) katika Kanda ya Ziwa Victoria, ujenzi wa soko la samaki la Mbamba Bay-Nyasa Mkoani Ruvuma, na kutangazwa kwa zabuni ya kupata Mkandarasi wa Ukarabati wa Soko la Samaki la Feriwa Dar es Salaam utakaoanza mwezi Julai 2021.

Vile vile anataja mafanikio mengine kuwa ni kutengwa kwa fedha za ndani shilingi bilioni 50 katika bajeti ya 2021/2022 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Mbegani Bagamoyo.

Waziri Ndaki anaendelea kusema kuwa Wizara imefanikisha kuzinduliwa kwa Dawati la Jinsia katika Sekta ya Uvuvi ili kuwawezesha wanawake kushiriki ipasavyo katika uchumi wa buluu kupitia Sekta ya Uvuvi pamoja na kanuni mpya za kusimamia na kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu zimetayarishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 334 ya tarehe 23 Aprili, 2021.

Lakini pia imetangaza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Sekta ya uvuvi kupitia mikutano ya kitaifa iliyojumuisha wageni kutoka Ufalme wa Saudi Arabia, Jamhuri wa Watu wa China, na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Aidha, hii ilifanikisha Juni 22, 2021 kwa mara ya kwanza Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) kukusanya jumla ya Dola za Marekani 800, 000 sawa na TSH 1.84 bilioni malipo ya leseni za uvuvi wa Bahari Kuu kwa meli 22 baada ya meli za kigeni kusitisha kuchukua leseni za Tanzania mwaka 2017/2018 kulikosababisha Serikali kukosa mapato na DSFA kushindwa kujiendesha yenyewe.

Aidha anasema ni katika kipindi hiki Wizara imefanikisha ununuzi wa maboti kumi na mbili (12) na injini sita (6) za kupachika kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi ambapo pia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI) imefanikiwa kuwawezesha wavuvi 100 katika ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi kuvua kwa ufanisi kwa kuwapatia taarifa za maeneo yenye samaki Baharini.

Waziri Ndaki anaeleza kwamba katika kipindi hiki DSFA pia ilikamilisha maandalizi na kuwezesha Mawaziri wenye dhamana ya Sekta ya Uvuvi SMT na SMZ kusaini Kanuni Mpya za Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu za mwaka 2021 na kuanza kutumika rasmi tarehe 23 Aprili, 2021.

Vile vile DSFA imeimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi na shughuli haramu zinazohusiana na uvuvi katika eneo la ukanda wa uchumi wa bahari (EEZ) inaloisimamia kwa kutumia mifumo yake ya kufuatilia mienendo ya meli ambapo ambapo tarehe 23 Aprili, 2021 ilinasa na kufanikisha kukamatwa kwa mashua Hg iliyokuwa ikipeperusha bendera ya Iran iliyokuwa na kilogramu 859.36 za madawa ya kulevya.

Anasema kwamba ili kunufaika na fursa za Uchumi wa Buluu kupitia tasnia ya ukuzaji viumbe maji, Serikali imetenga shilingi bilioni 18 ambazo zitatumika kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu katika vituo sita (6) vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji vya Mwamapuli-Tabora, Ruhila- Ruvuma, Kingolwira-Morogoro, Nyengedi - Lindi, Machui-Tanga, na Rubambagwe-Geita.

Anaeleza hatua hii itasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa vifaranga bora vya samaki kwa kuongeza uzalishaji kutoka vifaranga milioni 2 hadi kufikia milioni 8 kwa mwaka na kuboresha utoaji wa huduma za ugani hususani kutoa mafunzo kwa vitendo kwa angalau wananchi 3,000 ili kuhamasisha na kuwezesha ufugaji samaki na viumbe maji wengine kwa tija na faida na kupanua wigo wa huduma za ugani.

Lakini pia itasaidia kuanzisha mashamba darasa 40 ya ufugaji samaki yatayosimamiwa na vikundi vya vijana na kinamama.

Kwamba huu ni mwanzo wa utelekezaji wa azma ya kuwa shamba darasa katika kila halmashauri nchini ili kuhamasisha ufugaji wa samaki nchini kwa ajili ya kuboresha lishe, kuongeza kipato na kukuza uchumi.

Scanned with CamScanner

Habari Leo Uk.4
Julai 5,2021



Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Profesa Peter Msoffe (kulia) akipokea taarifa ya makabidhiano kutoka kwa aliyekuwa Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo, Masele Shilagi. Katikati ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji na Masoko (WMUV), Stephen Michael akishuhudia makabidhiano hayo yaliyofanyika kwenye ofisi za NARCO, Dodoma juzi. (Picha na Narco).

Scanned with CamScanner

Julai 5, 2021

mikubwa ya tafiti

# Wafugaji, wakulima walia na mpaka wa Pwani, Morogoro

NA WARIOBA IGOMBE, MOROGORO

JAMII ya wafugaji na wakulima wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro wameiomba serikali kuingilia kati changamoto ya mgogoro wa mipaka katika vijiji vinavyopakana na mikoa ya Morogoro na Pwani.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kuhusu mgogoro uliopo baina ya vijiji vinavyopakana na mikoa hiyo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Serengete B, wilayani Morogoro, Masudi Haji, alisema kwa muda mrefu wananchi wa kijiji hicho, wameshindwa kuendeleza ardhi yao kwa sababu ya migogoro ya mipaka.

"Mkulima au mfugaji katika kijiji hiki akiwa anafanya shughuli zake za kijamii kujipatia riziki, upande wa pili wa wananchi wa Pwani wanawazuia kufanya shughuli zao na kusababisha mgogoro kwa wananchi wa vijiji hivyo," alieleza.

Mwenyekiti huyo alibainisha kuwa changamoto hiyo ni ya muda mrefu na kwamba wananchi wa kijiji hicho wanaamini kwamba wao wapo Mkoa wa Morogoro.

Alisema vijiji vyenye changamoto

> **Mkulima au mfugaji katika kijiji hiki akiwa anafanya shughuli zake za kijamii kujipatia riziki, upande wa pili wa wananchi wa Pwani wanawazuia kufanya shughuli zao na kusababisha mgogoro kwa wananchi wa vijiji hivyo**
>
> Mwenyekiti wa Kijiji cha Serengete \B,wilayani Morogoro, Masudi Haji,

hiyo ni Gumba, Lugano na Kichemu huku akidai kuwa mpaka unaotambulika na wanakijiji wa vijiji hivyo ni ule uliopo kijiji cha Lukenge.

Miongoni mwa wakazi wa kijiji cha Kisemu, Mariam Shabani, alisema changamoto hiyo inachangia vijiji vyote vinavyopakana na Mkoa wa Pwani kushindwa kuwa na maendeleo, hivyo aliiomba Halmashauri ya Morogoro kutatua kero hiyo.

Mariam alieleza kuwa endapo hatua za haraka hazitachukuliwa kwa kuweka mipaka halali, kuna hatari ya watu kupoteza mali pomoja na maisha yao kwani migogoro ya ardhi.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alisema anatambua mgogoro huo na kwamba hatua za kuutatua inayofanywa na serikali ili kuitambua mipaka halisi, inashughulikiwa kisheria.

Msando aliwataka wananchi wa vijiji hivyo vilivyoko mpakani kuwa watulivu wakati serikali ikifanyia kazi suala hilo ambalo tayari lipo mikononi mwa Kamishna wa Ardhi.

Scanned with CamScanner

Mwananchi Uk.8
Julai 5,2021

**TUZO: PONGEZI**

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mifugo Profesa Elisante Ole Gabriel (kushoto), akimkabidhi cheti mtaalamu wa mifugo, Emmanuel Pangapanga, kwa kutoa huduma bora kwa wafugaji, wakati wa hafla ya utoaji tuzo iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Na Mpiga Picha Wetu




Scanned with CamScanner

# W'biashara Feri sasa kuhamishwa

Na Moshi Lusonzo

SERIKALI inatarajia kuwahamisha kwa muda wafanyabiashara katika soko la samaki la kimataifa la Feri jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kupisha kazi ya uboreshaji na ujengaji wa miundombinu ya kisasa.

Akizungumza na wadau wa sekta ya uvuvi baada ya kufanya ziara kwenye soko jana, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema ujenzi huo ambao utaanza mwezi ujao, unalenga kulifanya soko hilo kuwa bora zaidi katika uuzaji wa samaki katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Alisema mradi huo utaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 3, kati ya fedha hizo Sh. bilioni 1.7 zimetolewa na Benki ya Dunia.

Waziri Ndaki, alisema kazi ya uakarabati huo zitafanyika katika maeneo mawili ambayo ni kanda moja na mbili, ambazo wafanyabiashara wanafanya kazi katika mazingira magumu ya wazi.

"Tumeanza na kanda hizi mbili ambazo ni muhimu katika uzalishaji wa samaki, tunataka kuona kila bidhaa inayotoka hapa inakuwa na ubora wa kimataifa na hivyo kuongeza kipato kwa serikali," alisema.

Aliwaondoa wasiwasi wavuvi na wachuuzi kwamba hakuna atakayeathirika wakati wa ujenzi huo, kwani serikali haitawaondoa kabisa, na badala yake watahamishwa kwa muda kwenda sehemu zingine pembeni ya soko hilo.

Hakuna atakayeathirika katika zoezi hili, serikali inajua mpo hapa kwa ajili ya kutafuta kipato, tutachokifanya tutawapeleka kwa muda sehemu ya jirani ili mwendelee kuuza na kununua samaki," ameongeza kusema.

Hata hivyo, ametoa onyo kwa mkandarasi atakayepata kazi hiyo kukamilisha kazi ndani ya miezi saba kama ilivyoainishwa, kinyume chake hatakubali kuona kazi hiyo ikisuasua na kusababisha usumbufu kwa wafanyabiashara.

Mtaalamu wa ujenzi huo, Debora Sengusia, alisema mradi huo ambao utaanza Agosti mwaka huu baada ya kupatikana kwa mkandarasi, utakuwa shirikishi ili kuhakikisha kila mfanyabiashara wa soko hilo anatambulika na kupatiwa maeneo ya kufanyia kazi.

"Kama wataalamu tumejipanga kuhakikisha katika zoezi la kuhawamisha kwa muda na kisha kuwarudisha sehemu zao, hakuna atakayelalamika kwa kukosa eneo la kufanyia kazi," alisema Sengusia.

Scanned with CamScanner

# Bil 3.7/- kujenga masoko ya samaki

Na Oscar Job

SERIKALI itatumia zaidi ya Sh bilioni 3.7 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mialo na masoko kwa kuweka miundombinu ya kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi na kupunguza upotevu.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema hayo jana Dar es Salaam katika Mkutano wa Uongozi wa Soko la Samaki la Ferry, wavuvi na wafanyabiashara wa eneo hilo kuzungumzia maboresho ya soko hilo yanayotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Ndaki alisema ingawa idadi ya wavuvi inakadiriwa kufikia milioni 4.5 nchini, serikali imekuwa haipati pato la kutosha kutoka sekta hiyo.

Alisema wizara yake imejipanga kuweka mazingira rafiki ya kibiashara katika masoko yote na mialo ya kupokelea samaki ili kuongeza tija katika sekta ya uvuvi nchini.

"Lengo ni kuhakikisha tunawawezesha wavuvi kuongeza ufanisi na tija katika kazi yao sambamba na kuongeza mchango wao katika pato la taifa ambalo mwaka huu ni asilimia 1.7, tunakusudia siku zijazo hili likue zaidi," alisema Ndaki.

Alisema asilimia 95 ya wavuvi nchini ni wadogo wanaovua samaki kwa ajili ya matumizi ya chakula na asilimia tano iliyobaki wanavua kwa ajili ya biashara, hivyo serikali imeweka mkakati ili kuwainua.

"Rais Samia Suluhu aliilekeza wizara kuboresha mazingira na miundombinu ya uvuvi ili kuwawezesha wavuvi na wafanyabiashara kuchangia pato la taifa," alisema Ndaki.

Alisema asilimia 30 hadi 40 za mazao ya samaki yanapotea kutokana na kutokuwapo kwa miundombinu ya uhifadhi na kwamba, kufanyika kwa ukarabati huo kutawezesha samaki hao kuhifadhiwa kwa viwango bora.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija aliwataka wavuvi na wafanyabiashara kuushirikiana na mkandarasi ili akamilishe kazi hiyo kwa wakati.

Alisema ujenzi huo utakaofanyika kwa awamu utawalazimu wafanyabiashara hao kusogea kutoka maeneo ya ujenzi na kutengewa maeneo mengine hadi utakapokamilika ndiyo warejee.

Scanned with CamScanner